FUNZO LA 56

1. Mfano ni nini?
-Mfano ni hadithi inayofundisha ukweli wa Mungu.

2. Kwa nini Yesu alianza kufundisha watu kwa mifano?
-Kwa sababu watu wengi waliomfuata Yesu, hawakumwamini.

3. Katika mfano, mbegu ni nini?
-Mbegu ni Neno la Mungu.

4. Katika mfano , mpanzi ni nani?
-Mpanzi ndiye anayefundisha Maneno ya Mungu.

5. Ni watu gani walio kama njia?
-Mioyo ya watu hawa ni migumu.
-Neno la Mungu haliwezi kupenya ndani ya mioyo yao.
-Kisha, Shetani huja na kuchukua Neno la Mungu kutoka kwao.

6. Ni watu gani ambao ni kama mchanga wa miamba?
-Watu hawa wanasema kwamba wanaamini katika Mungu, lakini hawana imani chini yakutosha.

7. Ni watu gani walio kama udongo wenye miiba mingi?
-Watu hawa husema kwamba wanamwamini Mungu, lakini tamaa zao ni muhimu kwao kuliko Mungu.

8. Ni watu gani walio kama udongo mzuri?
-Watu hawa husikia Neno la Mungu, wanaamini kabisa, na huzaa matunda mengi.



-Yesu aliendelea kufundisha umati mpaka jioni.

-Kisha, Yesu na wanafunzi wake wakapanda mashua kuvuka ziwa la Galilaya.

Tusome Marko 4:35-37

35-Siku ile kulipokuwa jioni, akawaambia, Na tuvuke mpaka ng'ambo.
36-Wakauacha mkutano, wakamchukua vile vile alivyo katika chombo. Na vyombo vingine vilikuwako pamoja naye.
37-Ikatokea dhoruba kuu ya upepo, mawimbi yakakipiga chombo hata kikaanza kujaa maji.

-Walipokuwa wanavuka ziwa, nini kilitokea?
-Dhoruba kali ilikuja.

-Upepo ulikuwa unavuma kwa nguvu sana, na mawimbi yalikuwa juu sana hivi kwamba mashua ilikuwa katika hatari ya kuzama.

-Yesu alikuwa wapi?

Tusome Marko 4:38a

38-Naye mwenyewe alikuwapo katika shetri, amelala juu ya mto.

-Kwa nini Yesu alikuwa amelala?

-Kwa sababu Yesu alikuwa amewafundisha umati wa watu siku nzima, na alikuwa amechoka.

-Kwa nini Yesu alichoka?

-Ijapokuwa Yesu alikuwa Mungu kamili, pia alikuwa mwanadamu kamili.

-Kwa sababu mashua ilikuwa katika hatari ya kuzama, wanafunzi walifanya nini?

Tusome Marko 4:38b

38-Wakamwamsha, wakamwambia, Mwalimu, si kitu kwako kuwa tunaangamia?

-Wanafunzi walimwamsha Yesu.

-Wanafunzi walimwambia nini Yesu?
-"Je, hujali ikiwa tutazama?"

-Je, Yesu hakujali?
-Yesu alijali sana.

-Yesu alifanya nini?

Tusome Marko 4:39

39-Akaamka, akaukemea upepo, akaiambia bahari, Nyamaza, utulie. Upepo ukakoma, kukawa shwari kuu.



-Yesu alifanya nini?
-Yesu aliamuru upepo na bahari zitulie.

-Halafu nini kilitokea?
-Upepo ulitulia, na bahari ilikuwa tulivu kabisa.

-Je, Yesu aliwezaje kuamuru upepo na bahari zitulie?
-Kwa sababu Yesu alikuwa Mungu.

- Hapo mwanzo, ni nani aliyeumba upepo?
-Yesu.

-Hapo mwanzo, nani aliumba bahari?
-Yesu.

-Kwa nini upepo na bahari vilipaswa kumtii Yesu?

-Kwa sababu ni Yesu aliyeumba upepo na bahari.

-Yesu alisema nini baada ya upepo na bahari kutulia?

Tusome Marko 4:40

40-Akawaambia, Mbona mmekuwa waoga? Hamna imani bado?

-Yesu aliwauliza kwa nini hawakuwa na imani.

-Yesu alimaanisha nini?

-Yesu alikuwa akiwauliza kwa nini hawakuamini kwamba Yeye alikuwa Mungu.

-Ni nini basi wanafunzi walisema?

Tusome Marko 4:41

41-Wakaingiwa na hofu kuu, wakaambiana, Ni nani huyu, basi, hata upepo na bahari humtii?

-Ijapo wanafunzi walikuwa wamemwona Yesu akiwaponya watu, hawakuwa wamemuona Yesu akiamuru upepo utulie.

-Ijapo wanafunzi walikuwa wamemwona Yesu akiamuru mapepo yatoke kwa watu, walikuwa hawajawahi muona Yesu akiamuru bahari itulie.

-Hakuna kitu ambacho Yesu hawezi kufanya.
-Yesu ni Mungu.

-Baadaye, Yesu na wanafunzi wake walifika upande wa pili wa ziwa.

Tusome Marko 5:1-4

1-Wakafika ng'ambo ya bahari mpaka nchi ya Wagerasi.
2-Na alipokwisha kushuka chomboni, mara alikutana na mtu, ambaye ametoka makaburini, mwenye pepo mchafu;
3-makao yake yalikuwa pale makaburini; wala hakuna mtu ye yote aliyeweza kumfunga tena, hata kwa minyororo;



4-kwa sababu alikuwa amefungwa mara nyingi kwa pingu na minyororo, akaikata ile minyororo, na kuzivunja-vunja zile pingu; wala hakuna mtu aliyekuwa na nguvu za kumshinda.

-Je, yule mtu aliyepagawa na mapepo aliweza kujiokoa mwenyewe kutoka kwa nguvu za mapepo wote waliomdhibiti?
-La.

-Je, wengine waliweza kumwokoa mtu huyu kutoka kwa nguvu za mapepo yote waliomdhibiti?
-La.

-Wengine walikuwa wamejaribu kumsaidia kwa kumfunga.

-Lakini mapepo yaliyokuwa ndani yake yalikuwa na nguvu sana hata yakavunja minyororo ya chuma ambayo watu walikuwa wamemfunga nayo.

Tusome Marko 5:5

5-Na sikuzote, usiku na mchana, alikuwako makaburini na milimani, akipiga kelele na kujikata-kata kwa mawe.

-Je, tunajuaje kwamba mapepo hutuchukia sisi watu?

-Kwa sababu mapepo yalimlazimisha yule mtu kuishi kwenye mapango ambayo watu walizikwa.

-Kwa sababu mapepo yalimlazimisha yule mtu ajikate.

-Mapepo yalikuwa yamemfanya yule mtu kuwa mtumwa wao.
-Mapepo yalitaka mtu huyu ajiue.

-Kwa sababu mtu huyu alikuwa na mapepo wengi, walikuwa wakimuumiza sana.

-Lakini watu wote wamezaliwa kama mtu huyu, kwa sababu sisi sote huzaliwa kama watumwa wa mapepo.

-Ni nani mkuu wa mapepo yote?
-Shetani.

-Shetani na mapepo yake wanatuchukia sisi sote.
-Shetani na mapepo yake wanataka tu kutuangamiza sisi sote.

-Hata ikiwa Shetani na mapepo yake wanaonekana kutusaidia, wanafanya ili kutuangamiza.

-Maroho yanayodhibiti maisha yako yanaweza kuonekana kukusaidia.
-Ila yanafanya ili kukuangamiza.

-Shetani na mapepo wake wana kusudi moja tu maishani.
-Hiyo ni kuangamiza watu wengi kadri wawezavyo.

-Shetani na mapepo wake hawataki umjue Mungu na uokolewe kutoka kwa nguvu zao.

-Ilitokea nini wakati mtu huyu alipomwona Yesu?



Tusome Marko 5:6-7

6-Na alipomwona Yesu kwa mbali, alipiga mbio, akamsujudia;
7-akapiga kelele kwa sauti kuu, akasema, Nina nini nawe, Yesu, Mwana wa Mungu aliye juu? Nakuapisha kwa Mungu usinitese.

-Je, mapepo yalijua kwamba Yesu alikuwa Mungu Mwokozi?
-Ndiyo.

-Mapepo yaliogopa nini?

-Mapepo yaliogopa kwamba Yesu angeyapeleka kwenye Ziwa la Moto wa Milele.

-Ni nani aliye mkuu kuliko Shetani na mapepo yake?
-Yesu ambaye ni Mungu.

-Mungu atamtuma Shetani na mapepo yake katika Ziwa la Moto wa Milele wakati atakapotaka.

-Yesu aliambia nini mapepo?

Tusome Marko 5:8-10

8-Kwa sababu amemwambia, Ewe pepo mchafu, mtoke mtu huyu.
9-Akamwuliza, Jina lako nani? Akamjibu, Jina langu ni Legioni, kwa kuwa tu wengi.

10-Akamsihi sana asiwapeleke nje ya nchi ile.

-Je, mapepo yalijua kwamba hayakuweza kumshinda Yesu?

-Ndiyo.
-Yesu ana uwezo wote juu ya Shetani na mapepo yake.

-Mwishowe, Yesu atamtuma Shetani na mapepo yake yote katika Ziwa la Moto wa Milele.

-Kwa nini kutumikia maroho ambayo yatapelekwa na Mungu katika Ziwa la Moto wa Milele?

-Ni afadhali kumtumikia Mungu kuliko maroho.

-Yesu alifanya nini basi?

Tusome Marko 5:11-14

11-Na hapo milimani palikuwa na kundi kubwa la nguruwe, wakilisha.
12-Pepo wote wakamsihi, wakisema, Tupeleke katika nguruwe, tupate kuwaingia wao.
13-Akawapa ruhusa. Wale pepo wachafu wakatoka, wakaingia katika wale nguruwe; nalo kundi lote likatelemka kwa kasi gengeni, wakaingia baharini, wapata elfu mbili; wakafa baharini.
14-Wachungaji wao wakakimbia, wakaieneza habari mjini na mashambani. Watu wakatoka walione lililotokea.



-Kwa sababu mapepo yalimsihi Yesu, Aliwaruhusu kuingia kwenye nguruwe.

-Wakati nguruwe wote walikufa, je, mapepo yalikufa?
-La.

-Wakati nguruwe wote walikufa, kwa nini mapepo hayakufa?

-Kwa sababu mapepo ni roho.
-Kwa sababu mapepo hayana mwili kama watu au wanyama.

-Kwa nini Yesu hakuyatuma mapepo kwenye Ziwa la Moto wa Milele?

-Kwa sababu haikuwa wakati wa Mungu kuyaadhibu mapepo.

-Mwishowe, hata hivyo, Yesu atamtuma Shetani na mapepo yake wote katika Ziwa la Moto wa Milele.

-Watu ambao walikuwa wakiishi katika eneo hilo walipokuja, waliona nini?

Tusome Marko 5:15

15-Wakamwendea Yesu, wakamwona yule mwenye pepo, ameketi, amevaa nguo, ana akili zake, naye ndiye aliyekuwa na lile jeshi; wakaogopa.

-Je, yule mtu aliyekuwa amepagawa na mapepo alikuwa bado mtumwa wao?

-La.

-Ni nani aliyemweka huru huyo mtu kutoka kwenye kifungo cha mapepo?
-Yesu.

-Mtu huyo hakuwa mtumwa wa mapepo tena.
-Mtu huyo aliwekwa huru na Yesu, Mungu Mwokozi.

-Watu ambao walikuwa wakiishi katika eneo hilo walifanya nini?

Tusome Marko 5:16-17

16-Na wale waliokuwa wameona waliwaeleza ni mambo gani yaliyompata yule mwenye pepo, na habari za nguruwe.
17-Wakaanza kumsihi aondoke mipakani mwao.

-Kwa nini watu walimsihi Yesu aondoke?

-Kwa sababu watu walikuwa wapumbavu.
-Kwa sababu watu walikuwa wakifikiria zaidi nguruwe wao kuliko Mungu.

-Yesu, Mungu Mwokozi, alikuwa amekuja kuwaweka huru kutoka kwa Shetani, na walikuwa wakifikiria tu nguruwe zao.

-Leo, watu wengi ni kama watu hao.

-Watu wanafikiria zaidi juu ya nguruwe wao kuliko Yesu.



-Watu wanafikiria zaidi mali zao kuliko Yesu.

-Lakini nguruwe au mali zitakuweka huru kutoka kwa nguvu ya dhambi, mauti, na Shetani?
-La.

-Ni nini yule mtu aliyepagawa na pepo alimwambia Yesu?

Tusome Marko 5:18-20

18-Naye alipokuwa akipanda chomboni, yule aliyekuwa na pepo akamsihi kwamba awe pamoja naye;
19-lakini hakumruhusu, bali alimwambia, Enenda zako nyumbani kwako, kwa watu wa kwenu, kawahubiri ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana, na jinsi alivyokurehemu.
20-Akaenda zake, akaanza kuhubiri katika Dekapoli, ni mambo gani makuu Yesu aliyomtendea; watu wote wakastaajabu.

-Kwa nini Yesu hakumruhusu yule mtu aende naye?

-Kwa sababu Yesu alitaka aambie familia yake na wengine kile Mungu alikuwa amemfanyia.

-Wakati Mungu anatuweka huru kutoka kwa nguvu za Shetani na mashetani wake, ni vizuri kuwaambia wengine kuwa Mungu pia anataka kuwaokoa kutoka kwa uovu.